MANYAM FRANCHISED TESTS

Std Six | Mar-14 | Kiswahili | 001

NAME.....SCHOOL.....DATE.....

Muda: Saa 1 dakika 40

<u>Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 10. Chagua neon lifaalo zaidi ya yale uliyopewa.</u>

Wanafunzi ___1___ walijiandaa kuufanya ___2___wao ___3___muhula wa kwanza. Niliingiwa na wasiwasi ___4___ sikuwa nikidurusu mara kwa mara. ___5___ nilijipa moyo. Nilitamani kumpiku aminata japo yeye ni bingwa darasani. Alikuwa mwanafunzi mzuri __6___mimi. Kwa mara __7___, tukaamua kudusuru katika makundi ___8___. Tulishirikiana kwa kuwa umoja ni ___9___utengano ni udhaifu. Maswali ___10___rahisi

	A	B	C	D
1.	Sote	wote	yote	zote
2.	Mtihani	mtahini	mtahiniwa	kazi
3.	Ya	za	wa	la
4.	Ili	kwa nini	sababu	kwa sababu
5.	Hata hivyo	hata	kwa hivyo	na hivyo
6.	Kuniliko	kuliko	kumliko	kuwaliko
7.	Jingine	mengine	nyingine	zingine
8.	Chetu	zetu	letu	yetu
9.	Nguvu	nguzo	gumzo	mbaya
10.	Ilikuwa	yalikuwa	ulikuwa	yalikua

___11___?" nilimsalimu babu yangu. Alishangaa nilipomwambia kuwa magari ___12___ ___13___ katika ajali mbaya ___14___. Abiria waliaga ___15___ huzuni nyingi.

	A	B	C	D
11.	Shikamoo	habari	marahaba	sasa
12.	Tatu	matatu	mbili	tano
13.	Yaligongana	ziligongana	yaliegezwa	zilianguka
14.	Barabarani	ofisini	darasani	mtoni
15.	Kwa kuwa	bila	na	kwa

Kutoka swali 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi

16. Wingi wa 'kitabu change kimeanguka' ni
    A. Vitabu vyangu vimeanguka
    B. Vitabu vyetu vimeanguka
    C. Vitabu zangu zimeanguka
    D. Vitabu chetu vimeanguka
17. Kamilisha tasbihi, mrefu kama,
    A. Twiga
    B. Nyundo
    C. Makaa
    D. Kinyonga
18. Chagua kiwakilishi kifaacho kukamilisha sententsi
    Farasi ___ni wa Onyango
    A. Hii
    B. Wao
    C. Huyu
    D. Hivi
19. Tegua kitendawili hiki
    Mama nieleke
    A. Motto
    B. Kitanda
    C. Shuka
    D. Blanketi
20. Andika kinyume cha sentensi hii
    Bibi alivua nguo kabla ya kuoga
    A. Nyanya alivua nguo kabla ya kuoga
    B. Baba alivaa nguo kabla ya kuoga
    C. Babu alivaa nguo kabla ya kuoga
    D. Baba alifaa nguo kabla ya kuoga
21. Huu mchoro ni wa umbo lipi?
    A. Pia
    B. Kikokmbe
    C. Kopa
    D. Mche
22. Chagua sentensi sahihi
    A. Mburukenge amesimama nyuma ya gari
    B. Mburukenge imesimama nyuma ya gari
    C. Zulia imetandikwa sakafuni
    D. Kabati yetu imetengenezwa
23. Ni kiungo kipi cha mwili wa binadamu ambacho hutumika kuingiza hewa safi na kutolea hewa chafu mwilini
    A. Moyo
    B. Roho
    C. Pafu
    D. Figo
24. Chagua kihusishi katika sentensi ifuatayo___

    Mwalimu wetu amesimama kando ya gari

    A. Wetu
    B. Kando ya
    C. Amesimama
    D. Ya
25. Dada ya mama huitwa___
    A. Halafi
    B. Mjomba
    C. Shangazi
    D. Amu
26. Mchoro huu wa saa unaonyesha saa ngapi?
    A. Saa kumi na mbili na dakika ishirini na tano
    B. Saa sita na dakika ishirini na tano
    C. Saa tano na dakika kumi na mbili
    D. Saa sita na dakika tano
27. Chagua neon mwafaka kukamilisha sentensi hii___
    Karanja ____alicheza kandanda
    A. Mwenye
    B. Wenyewe

C. Mwenyewe
D. Enyewe

28. Kofia ya Kiswahili ivaliwayo na wanaume huitwa___
    A. Bulibuli
    B. Kaptura
    C. Kanzu
    D. Kanchiri
29. Kamilisha sentensi
    Mbwa _____swara
    A. Walimkimbisha
    B. Walikimbizana
    C. Walimkimbisa
    D. Walikimbiswa
30. Tarakimu; watoto (2/3) katika darasa ni wavulana. Kwa maneno ni
    A. Nusu
    B. Thuluthi tatu
    C. Thuluthi mbili
    D. Robo

Soma kifungu kifuatacho kasha

Wasanii wa humu nchini wanaendelea kunufaika hasa katika sanaa ya uimbaji kuliko watunzi wa mashairi. Watu wengi wanaoamini kuwa kutunga mashairi ni kazi rahisi lakini wanapoketi na kujaribu, wanashindwa kuandika angalau ubeti moja wa shairi. Utunzi wa mashairi umeingiliwa na walaghai. Kwa kweli tungo zimo hatarini.

Utunzi wa mashairi hufuata kanuni au sharia maalum. Mtunzi sharti awe mtu anayeijua lugha kwa mapana na marefu nan i gwiji wa sanaa hii. Mshairi hutumia lugha kwa njia ya kipekee kutoa ujumbe wake. Wakati mwingine hufupisha au kurefusha maneno, ili kulenga mtriririko wa mizani na vina.

Washairi huonyesha uzalendo kwa kuisifu nchi yao bila kuikashifu.

Katika shairi, uzito wa mawazo ni muhimu zaidi. Hata hivyo, mashairi ya aina ya tarbia yapendwa na watunzi wengi kuliko tathlitha na takhmisa. Mimi hupendezwa zaidi na mashairi ya ngojera hasa watu wawili wanapohusika kuyakariri.

31. Wasanii wengi wananufaika na sanaa ya___
    A. Uchoraji
    B. Uimbaji
    C. Mashairi
    D. Uchongaji
32. Kwa nini watu wengi wanashindwa kutunga mashairi?
    A. Hayana sharia
    B. Ni rahisi
    C. Mtunzi sharti aifahamu lugha
    D. Ni magumu sana
33. Mtu anayetunga mashairi huitwaje?
    A. mwimbaji
    B. topasi
    C. malenga
    D. mlaghai
34. mtunzi wa mashairi ana uhuru wa kurefusha au kufupisha maneno ili
    A. kukamilisha ubeti
    B. kumaliza mshororo
    C. kuifanya shairi gumu
    D. kutosheleza idadi ya vina au mizani
35. mwandishi anasema tungo zimo hatarini. Unafikiri ni kwa nini?
    A. Hapendi tungo
    B. Zimeingiliwa na walaghai
    C. Hazina magwiji
    D. Watu wengi wanpenda uimbaji

36. Mwandishi anapenda aina gani ya mashairi?
    A. Tarbia
    B. Takhmisa
    C. Tathlitha
    D. Ngojera
37. Washairi huonyesha uzalendo kwa nchi yao kwa njia gani?
    A. Kuisifu nchi
    B. Kuikashifu nchi
    C. Kuimba nchi
    D. Kuilaani nchi
38. Ni aina ipi ya mashairi inayopendwa na watunzi wengi wa mashairi?
    A. Tarbia
    B. Ngojera
    C. Tkhmisa
    D. Tathlitha
39. Kitu muhimu zaidi katika shairi ni
    A. Mizani
    B. Vina
    C. Ubeti
    D. Uzito wa mawazo
40. Kulingana na kifungu
    A. Mashairi hayapendwi
    B. Watunzi wa mashairi wanaendelea kunufaika
    C. Kutunga mashairi si kazi rahisi
    D. Mashairi hutungwa na magwiji pekee

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali 41-50

Ufanisi wa taifa hutegemea mchango na juhudi za kila mwananchi. Lakini baadhi yetu tuna fikra mbovu kuwa kunao watu wanaostahili kuiendeleza nchi yetu. Wanataka serikali iwafanyie kila kitu. Hawatajiuliza wanachofanyia nchi yetu. Tunahitaji kuwa na bidii kama za mchwa na tume na umoja wa nyuki ili tufanikiwe.

Wanafunzi wanalo jukumu kwa taifa; kuchangia maendeleo ya nchi kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za shule. Wajibidiishe sio tu katika shughuli za masomo pekee lakini pia katika michezo kama kandanda, riadha na uigizaji. Kwa kufanya hivyo utakuza utamaduni wetu na kuiendeleza nchi. Isitoshe, unaweza kushiriki katika shughuli za upandaji miti na kuzoa taka ili kuyanadhifisha mazingira yetu.

Baada ya masomo, si muhimu kuhamia mjini kutafuta kazi zenye donge nono. Mashamba yakiachiwa wazee, mazao yatakuwa haba na watu watakabiliwa na baa la njaa. Kufanikiwa masomoni ni muhimu lakini iwapo elimu uliyoipata haiwezi kukusaidia kuvumba mbinu za kuiendeleza taifa, basi yote ni bure.

41. Ufanisi wa taifa unahitaji
    A. Kushughulika kila mara katika upanzai wa miti
    B. Ushirikiano wa kila mwananchi
    C. Kutotarajia serikali kufanya lolote
    D. Serikali kutufanyia kila kitu
42. Kulingana na kifungu, watu wenye fikira mbovu
    A. Wana bidii za mchwa na ushirikiano wa nyuki
    B. Wanangoja serikali ifanye kila kitu
    C. Huokota taka na kupanda miti
    D. Wanashirikiana
43. ‘kuwa na bidii kama za mchwa’ ni fani gani ya lugha?
    A. Methali

B. Nahau
C. Kitendawili
D. Tashbihi

44. ‘kazi zenye donge nono’ maana yake ni
A. Zenye mishahara mikubwa
B. Zenye mishahara midogo
C. Zenye watu wanene
D. Zilizo mbaya

45. Wanafunzi wanastahili kujibadilisha katika mambo yafuatayo ila
A. Masomo
B. Michezo
C. Kunadhifisha mazingira
D. Wizi

46. Maana ya ‘mazao yatakuwa haba’ ni
A. Yatakuwa machache
B. Yatakuwa mengi
C. Hayatakuwepo
D. Yataangamizwa

47. Elimu yako masomoni itakuwa bure iwapo
A. Utavumbua mbinu za kuiendeleza taifa
B. Matokeo yako yatakuwa mazuri
C. Utashindwa kuvumbua mbinu za kuiendeleza taifa
D. Hautashirikiana na wenzako

48. Methali inayoweza kujumuisha kifungu hiki ni
A. Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu
B. Dawa ya moto ni moto
C. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
D. Motto umleavyo ndivyo akuavyo

49. Ni sentensi ipi sahihi?
A. Uigizaji hukuza utamaduni
B. Michezo si muhimu
C. Mazingira yachafuliwe
D. Masomo si muhimu

50. Kichwa kifaacho habari hii ni
A. Kazi
B. Utamaduni
C. Michezo
D. Maendeleo ya taifa

Answers

1. **B**
2. **A**
3. **C**
4. **D**
5. **A**
6. **B**
7. **C**
8. **D**
9. **A**
10. **B**
11. **A**
12. **B**
13. **A**
14. **A**
15. **D**
16. **B**
17. **A**
18. **C**
19. **B**
20. **C**
21. **A**
22. **A**
23. **C**
24. **B**
25. **C**
26. **A**
27. **C**
28. **A**
29. **A**
30. **C**
31. **B**
32. **C**
33. **C**
34. **D**
35. **B**
36. **D**
37. **A**
38. **A**
39. **D**
40. **C**
41. **B**
42. **B**
43. **D**
44. **A**
45. **D**
46. **A**
47. **C**
48. **A**
49. **A**
50. **B**

Manyam Franchise all rights reserved-Tel 0728450425 email: sales@manyamfranchise.com